**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

# MWALIKO WA ZABUNI

**Kwa ajili ya:**

## KUPANGA NA KUENDESHAJI KITUO CHA MAFUTA KINACHOMILIKIWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE ENEO LA TUKUYU MJINI

**Tarehe: 29.09.2025**

1. **Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe** inawakaribisha mtu binafsi, Kampuni, na Taasisi kwa ajili ya kuomba Zabuni ya Kupanga na Kuendesha Kituo cha Mafuta ya Magari na Mitambo. Kituo hicho kinamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe na kipo eneo la Tukuyu Mjini kandokando ya barabara ya kwenda Kyela.

2. Mwombaji unakaribishwa kuleta zabuni yako **ya bei** kwa ajili ya ununuzi wa Zabuni kama ilivyoelekezwa kwenye kitabu cha Zabuni.

3. Mwombaji mwenye nia na uwezo anaweza kufanya ziara ya kutembelea na kukagua eneo hilo ili kujua mahali Kituo kilipo kwa gharama zake tarehe 02.10.2025 Saa 04:00 Asubuhi Baada ya hapo kutakuwa na kikao cha awali cha zabuni "Pre-bid meeting" kitakachofanyika katika Ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe muda ni saa 08:00 Mchana ili maelekezo Zaidi ya namna ya kupanga na kuendesha Kituo hicho.

4. Vitabu vya zabuni vitakuwa kwa Lugha ya **Kiswahili na** vitanunuliwa na mwombaji anayehitaji kwa gharama ambayo haitarudishwa ambayo ni Shilingi za kitanzania TSH.500,000/= (Laki tano tu) taslimu. Fedha hizo zilipwe Halmashauri ya Rungwe Ofisi ya Mapato. Vitabu vya zabuni vitatolewa Halmashauri ya wilaya ya Rungwe ofisi ya Ununuzi ghorofa ya Pili kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka 9:30 alasiri kwa siku za kazi tu.

5. Zabuni zote ziwe na nakala **halisi** (original) moja na **nakala** (Copy) moja inayofanana, iliyojazwa kwa usahihi na iliyowekwa kwenye bahasha iliyofungwa kwa lakiri na zitapokelewa na kuwekwa kwenye sanduku la zabuni. Bahasha ziandikwe "**Zabuni kwa ajili ya Kupanga na Kuendesha Kituo cha Mafuta kinachomilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kilichopo eneo la Tukuyu Mjini**"na kuwasilishwa kwa mkono kwa Anuani ifuatayo;

**Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe,**
**Katibu wa Bodi ya Zabuni,**
**Ofisi ya Manunuzi,**
**S.L.P 148**
**RUNGWE.**

9. Mwisho wa kuwasilisha zabuni ni Siku ya Jumatano **Tarehe** 08.10.2025 **kabla ya Saa 04:00 Asubuhi** Zabuni zote zitafunguliwa hadharani Tarehe 08.10.2025 Saa 04:00 Asubuhi mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya

wawakilishi wa wawekezaji au wawekezaji walioamua kuhudhuria katika kikao katika Ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ghorofa ya pili.

6. Zabuni zote lazima ziambatanishwe na tamko la kinga ya zabuni (Tender Securing Declaration) kwa mpangilio ulioelekezwa katika nyaraka za zabuni.

7. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya Zabuni, Zabuni za kielektroniki, na Zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa Zabuni, kwa hali yoyote ile hazitakubaliwa kwa tathimini.

.......................

Mchau R,B.

**MKURUGENZI WA MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE